- Serikali iridhie Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 2007.
- Serikali za Mitaa ziendelee na jukumu la kuwaainisha watu wenye ulemavu walio kwenye maeneo yao na kuweka mipango inayotekelezeka ya kuwasaidia.
- Serikali iimarishe Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambao uko chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii kwa kuupatia fedha za kutosha ili uweze kuendesha shughuli zake za kuwasaidia watu wenye ulemavu kama zilivyoainishwa kwenye sheria mpya ya watu wenye ulemavu.
- Sheria mpya iitambue Serikali pamoja na sekta binafsi kama waajiri wanaotakiwa kuzingatia haki za watu wenye ulemavu wakati wa kutoa ajira na haki zao mahali pa kazi.
- Wamiliki wa vyombo vya habari wahakikishe habari zinazorushwa kwenye vyombo vya habari zinatolewa kwa kuzingatia hali za watu wenye ulemavu.
- Serikali ifanye sensa kwa nchi nzima ili kubaini idadi ya watu wote wenye ulemavu na aina za ulemavu wao ili kupata takwimu sahihi ya idadi yao na kujua jinsi ya kutekeleza upatikanaji wa haki zao.

Serikali iliyazingatia mapendekezo hayo na kupelekea kutungwa kwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2009.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

## HITIMISHO

Hali ya ulemavu katika jamii ya Watanzania imekuwa ikichukuliwa kama maradhi au laana na hivyo kuwachukulia watu wenye ulemavu kama wagonjwa au wenye bahati mbaya. Mtazamo huu umesababisha ionekane kwamba watu hao wanahitaji matibabu au msaada ili waweze kumudu maisha yao. Lakini mtazamo huo si sahihi, muda umefika sasa kwa jamii ya Watanzania kubadilika na kuichukulia hali ya ulemavu kama ni maumbile tofauti. Suala la ulemavu kwa sasa hivi ni la haki za binadamu zaidi na si maradhi wala kuhitaji msaada.

Huu ni muda muafaka kwa Serikali kuhakikisha kwamba, masuala ya watu wenye ulemavu yanapewa kipaumbele katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa vile masuala hayo ni mtambuka, na hasa ikizingatia kuwa Tanzania ni kati ya nchi ambazo zilishiriki kwa karibu sana kukamilisha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu, 2007 na kuridhia Mkataba huu.

**Mawasiliano:**

Katibu Mtendaji,

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,

Mtaa wa Luthuli, Kiwanja Na. 8,

S.L.P. 3580

**DAR ES SALAAM – TANZANIA.**

Simu: +255 22 2123533

Faksi: +255 22 2123534

Barua Pepe: lrct@lrct-tz.org

Tovuti: www.lrct-tz.org

© LRCT 2010

Printed By Rainbow Printers, Email: info@rainbowprinters.co.tz

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**




# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

## *ELIMU YA SHERIA KWA UMMA*



# HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU TANZANIA

## UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ni Idara inayojitegemea iliyoanzishwa na Sheria ya Bunge Na. 11 ya 1980, Sura 171 [Toleo la 2002]. Sheria hii inaipa Tume mamlaka ya kufanya mapitio ya sheria na kisha kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo ambayo huwasilishwa kwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria. Lengo la Tume ni kuzifanya sheria za nchi ziende sanjari na mazingira ya sasa ili kudumisha utawala wa sheria na usimamizi wa haki nchini. Aidha, Tume inaweza kufanya utafiti na kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya iwapo inaona kuna haja ya kufanya hivyo. Tangu Tume ilipoanza shughuli zake mwaka 1983, imetoa Taarifa mbali mbali zinazopendekeza marekebisho ya sheria ikiwa ni pamoja na Sheria zinazowahusu Watu wenye Ulemavu.

## DHUMUNI LA KUFANYA UTAFITI WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mnamo mwaka 2006, Tume iliamua kufanya utafiti ili kuupitia mfumo wa sheria juu ya haki za watu wenye ulemavu ili kubaini vikwazo na matatizo yanayowakabili katika nyanja mbalimbali. Tume ilifikia uamuzi huo kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na maazimio, matamko na mikataba mbalimbali ya kimataifa inayosisitiza umuhimu wa nchi wanachama kutambua na kutoa kipaumbele kwa haki muhimu za watu wenye ulemavu. Hii ni pamoja na Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Watu wenye Mtindio wa Ubongo la mwaka 1971 na Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Watu wote wenye Ulemavu la mwaka 1975.

Umuhimu wa kufanya utafiti huo ulitokana na sera mbalimbali za nchi ambazo zinaelekeza na kusisitiza umuhimu wa kutambua haki za watu wa aina hiyo katika nyanja zote za kijamii kwa mfano; Sera ya Taifa ya Walemavu ya mwaka 2004 pamoja na Sera

*Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,*

ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 inayosisitiza usawa wa elimu kwa watu wote.

Pamoja na sera nzuri, Sheria ya Ajira ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 1982 na Sheria ya Matunzo na Hifadhi ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 1982 zilikuwa na upungufu mwingi. Upungufu huo ulitokana na kutungwa kwa sheria hizo miaka mingi iliyopita wakati hakuna sera zozote kama ilivyo hivi sasa. Sheria hizo mbili za watu wenye ulemavu ziliwachukulia walemavu kama wagonjwa ambao wanahitaji matibabu au msaada wa matunzo na hifadhi na si kuwawezesha au kuwaondolea vikwazo vinavyowakabili ili wafanye kazi zao wenyewe.

Aidha, sheria hizo mbili zilijikita zaidi kwenye masuala makubwa mawili ambayo ni upatikanaji wa ajira na kupatiwa msaada wa matunzo au hifadhi kwenye makazi maalumu ya watu wenye ulemavu. Lakini, mtazamo wa sheria hizo kwa sasa haukubaliki na vilevile masuala ya watu wenye ulemavu ni zaidi ya ajira, matunzo na hifadhi.

## MTAZAMO WA SERIKALI NA JAMII KUHUSU HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU

Wakati wa utafiti, Tume iliwashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu, vyama vya watu wenye ulemavu pamoja na Taasisi za Serikali.

Utafiti huo ulibaini kwamba, pamoja na sheria mbili za mwaka 1982 za watu wenye ulemavu kuwa na upungufu mwingi, kuna vikwazo vingine vingi vya kiutendaji kama vile:-

- ❖ Kutokuwa na taarifa sahihi juu ya haki za watu wenye ulemavu kwa watendaji wa Serikali na hivyo kusababisha suala zima la kutambua na kutekeleza haki za watu wenye ulemavu kuwa gumu;

*Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,*

- ❖ Kuwepo kwa miundombinu isiyozingatia hali za watu wenye ulemavu hivyo kushindwa kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kijamii kama vile siasa, michezo na kupata habari;
- ❖ Kutokuwa na uelewa wa sheria za watu wenye ulemavu za mwaka 1982 zinazohusu maslahi yao hivyo kushindwa kudai haki zao;
- ❖ Serikali kutokuwa na mpango madhubuti wa kuhakikisha masuala ya watu wenye ulemavu yanaingizwa kwenye kila sekta kwa vile ni masuala mtambuka;
- ❖ Watu wenye ulemavu kukabiliwa na umasikini na unyanyapaa kwa sababu ya mila potofu zilizojengeka kwenye jamii dhidi yao na hivyo kupelekea kukosa haki zao za kimsingi kama vile elimu na ajira;
- ❖ Kushindwa kumudu gharama za vifaa au vitendea kazi vya kuwasaidia kupunguza athari za ulemavu wao wanapokuwa kwenye shughuli mbalimbali za kijamii;
- ❖ Idara ya Ustawi wa Jamii kukabiliwa na ufinyu wa Bajeti.

## MAPENDEKEZO YA TUME KWA SERIKALI

Tume ilipendekeza maboresho mbalimbali kwa ajili ya kuondoa udhaifu na kurekebisha upungufu ambao ulibainika wakati wa utafiti. Mapendekezo hayo ni kama yafuatayo:

- ❖ Kufuta sheria mbili za mwaka 1982 za watu wenye ulemavu na badala yake kutungwa kwa sheria moja ya watu wenye ulemavu ili kusimamia masuala yao mbalimbali.